




**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWA**



30/09/2024

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUKANUSHA TAARIFA INAYOSAMBAA MITANDAONI KUHUSU KIWANDA CHA  
KOROSHO KISARAWA**

Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe inapenda kuujulisha umma kupuuzia taarifa zinazosambaa katika Mitandao ya kijamii zinazohusisha baadhi ya watumishi wa Halmashauri kugawana kiasi cha fedha Tsh 448,800,000/= (Milioni Mia Nne, Arobaini na Nane na Laki Nane) kwa kumlipa Mkandarasi **MOHAMED BUILDERS LTD** bila kuwa na Mkataba.

Ukweli ni kwamba; Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe iliingia Mkataba na Mkandarasi wa Kampuni ya **MOHAMED BUILDERS LTD** ya S. L. P 38439 Dar es Salaam tarehe 18 Mei, 2023 kwa ajili ya Ujenzi wa Kiwanda cha Korosho katika Kijiji cha Vilabwa Kata ya Mzenga ukiwa na thamani ya **Shs 2,992,589,543.53** Mkataba huo ulikuwa wa mwaka mmoja, kupitia tenda namba **LGA/009/HQ/2022/2023/CASHEW/W/119**.

Baada ya Mkandarasi kuoneshwa eneo la ujenzi alilipwa malipo ya awali (Advance Payment) kiasi cha Tsh. **448,888,431.53**, kulingana na kifungu No 36 'Clause' 57.1 kinachotamka kuwa "Mkandarasi atalipwa 15% ya gharama ya Mkataba". Mkandarasi alimwandikia barua Mkurugenzi Mtendaji (W) tarehe **24 Novemba, 2023** yenye Kumb Na. **MBL/KISARAWA/231124/A** akiomba kupatiwa nyaraka zote zinazohusiana na Mradi ikiwemo michoro ya Kihandisi ili aanze ujenzi wa kiwanda hicho,

Baada ya kupokea barua hiyo na kujiridhisha na mapungufu yaliyokuwepo katika Mkataba wa awali Halmashauri ilifuata hatua zote za marekebisho kwa kufuata taratibu zote za Manunuzi, kwa sasa marekebisho ya Mkataba wa awali yapo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kufanyiwa upekuzi ili idhini ya kusaini iweze kutolewa.

Na Mwisho Mkandarasi huyo alisharipoti eneo la mradi na baadhi ya kazi zimeshaanza.

**Taarifa hizo zenye lengo la kuichafua Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe Zipuuzwe.**

TAARIFA HII IMETOLEWA NA;

Farijala J. Kimaro

**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWA**